TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo, Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Ref.No: Taro /P/2022/ A01 Date: 3rd February 2022

**MTAZAMO WA KISHERIA KUHUSU MIALIKO YA KUHUDHURIA UZINDUZI WA TUZO ZA MUZIKI TANZANIA**

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Mnamo tarehe 28 Januari 2022, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) likishirikiana na Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) walifanya Uzinduzi wa Tuzo za Muziki Tanzania. Shughuli hiyo ilihudhuliwa na wadau mbalimbali wa muziki wakiwemo wasanii mbalimbali wa muziki. Maswali ya sintofahamu yaliibuka kwa baadhi ya wasanii waliokosa mialiko ya kuhudhuria uzinduzi huo. Sintofahamu hizo zilijikita katika maswali mawili makuu kama yalivyoainishwa hapo chini.

i. Wasanii wa muziki waliohudhuria uzinduzi walialikwa kwa kuzingatia vigezo gani?
ii. Wasanii wa muziki wasiohudhuria walikosa mialiko kwa kuzingatia vigezo gani?

Maswali hayo mawili yalijibiwa na mahojiano ya waandishi wa habari yaliyofanywa na Kaimu Katibu Mtendaji wa BASATA, **Bwana Matiko Mniko** mchana kabla ya uzinduzi, na mahojiano mengine ya waandishi wa habari na Katibu Mkuu wa Shirikisho la Muziki Tanzania (Bwana Farid Kubanda-FID Q) jioni wakati wa uzinduzi huo.

**Mahojiano ya Kaimu Katibu Mtendaji wa BASATA, Bwana Matiko Mniko na Mtangazaji wa kipindi cha XXL (Clouds Fm) aitwaye Mamy Baby- NUKUU**

**Mwandishi Mamy Baby:** "... Ni vigezo gani vilitumika kuwainvite wale artists leo kwenye uzinduzi wa tuzo?"

**Bwana Matiko Mniko:** "……tuna mashirikisho, shirikisho la muziki lipo, lakini kuna vyama vipo chini ya shirikisho la muziki, kuna vyama saba kwa hiyo wadau wetu wote mawasiliano au mialiko wanapata kupitia hizo channels…"

**Mahojiano ya kundi la waandishi wa habari na Katibu Mkuu wa Shirikisho la Muziki Tanzania (Bwana Farid Kubanda-FID Q) jioni wakati wa uzinduzi huo-NUKUU**

**Mwandishi:** "…..**Wakazi** anasema kwamba ye hakualikwa kwa hiyo hajapendezwa na kitu kama hicho"

ANGALIZO: **WAKAZI** ni msanii wa muziki wa kizazi kipya miondoko ya kufoka (Hip Hop)

**Bwana Farid Kubanda-FID Q:** "...wao walichoangalia zaidi kwamba waliangalia watu ambao wamejisajili COSOTA. Sijui umenielewa vizuri kwa hiyo wasanii wengi sana ambao hawajaalikwa leo ni kwasababu wengi wao hawajajisajili COSOTA ukiachilia swala la ukumbi wetu wa leo kuonekana mdogo…."

**<u>HOJA YA KISHERIA</u>**

**Je kutokujisajili COSOTA kunamfanya msanii wa muziki kupoteza haki zote za kunufaika na shughuli za Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COPYRIGHT SOCIETY OF TANZANIA-COSOTA)?**

COSOTA imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 46 cha sheria iitwayo Copyright and Neighbouring rights Act. No.7 of 1999 (Cap.2018.R.e. 2002). Kifungu cha 47 kifungu kidogo (a) kimeipa COSOTA kazi ya kuamasisha na kulinda maslahi ya wabunifu ikijumuisha wasanii wa muziki. Sheria hiyo mama ya Hakimiliki, haijaeleza popote kuwa msanii akiwa hajasajiliwa na COSOTA basi anapoteza haki zote za kunufaika na shughuli zote za COSOTA.

LAKINI, Sheria imeagiza kuwa, kuna baadhi ya huduma ili msanii azipate COSOTA, anahitajika kujisajili COSOTA. Huduma hizo zimeoanishwa na sheria. Mfano;Upokeaji wa mirabaha. Msanii wa muziki kuhudhuria Uzinduzi wa Tuzo za muziki sio sehemu ya huduma hizo na ahitaji usajili

Kwa mujibu wa Kanuni ya **3** ya Kanuni ziitwazo **The Copyright And Neighbouring Rights (Registration Of Members And Their Works) Regulations**, **2005. GN. NO.6 OF 20 January 2006**, na marekebisho yake yaani **The Copyright And Neighbouring Rights (Registration Of Members And Their Works) Regulations**, 2013 GN.NO.413 OF 2013, Inaelekeza kwamba Mbunifu au Mmiliki wa Hakimiliki anaweza kufanya maombi ya kuwa mwanachama wa

COSOTA. Nukuu maneno ya sheria ***" An author or other owner of copyright may apply for membership of COSOTA"***

Sheria hiyo iko wazi kabisa, Msanii kujisajili COSOTA ni maamuzi yake ya hiari. Pia haijalazimisha popote pale Msanii kujisajili COSOTA. **KWA HIYO**, Usajili usitumike kama sababu ya kuwabagua na kuwanyima wasanii haki zao kwenye shughuli ambazo haziitaji usajili

Ukirejea ibara ya 13(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977(Kama inayvofanyiwa marekebisho mara kwa mara) inaamuru kuwa;-

***"Ni marufuku kwa mtu yoyoye kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi***"

***HITIMISHO***

Kitendo cha makusudi kilichofanywa na COSOTA na BASATA kuwanyima fursa wasanii mbalimbali wa muziki kuhudhuria Uzinduzi wa Tuzo za Muziki kwasababu hawajasajiliwa COSOTA ni **UBAGUZI WA WAZIWAZI** kinyume na sheria za nchi na pia ni kinyume na Katiba ya nchi. COSOTA na BASATA Wanapaswa kuomba radhi kwa UMMA ulioumizwa na uovu huo.

Kitendo cha COSOTA kushindwa kulinda maslahi ya wasanii wa muziki mpaka wanabaguliwa ni kuacha kutekeleza majukumu yao kama ilivyoelezwa na sheria. COSOTA wanapaswa kuomba radhi kwa UMMA ulioumizwa.

Uzinduzi wa Tuzo za Muziki ulipaswa kufanywa kama shughuli nyingine za umma (matamasha ya umma/yale yasiyo na viingilio/matamasha ya bure) ili kuwawezesha wasanii wote wa muziki kufurahia haki yao bila KUBAGULIWA.

TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

ASANTENI
MUNGU AIBARIKI TANZANIA
MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA
(Kazi iendelee)

Wako Mtiifu

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**